# Utamaduni wa Usomaji Tanzania

*Mugyabuso M. Mulokozi*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

*... books can teach us, can inspire us, or can refresh our minds with the pleasure of a good story well told. Books can break down the isolation of our lives and provide us with a friend wherever we may be...*

J.K. Nyerere *"The Importance and Pleasure of Reading" in* Freedom and Socialism *(OUP Dar 1968) uk.108.*

* * *

Vitabu ni hazina ya akili na elimu. Hazina ya fedha, dhahabu na majohari hufunguliwa kwa funguo. Ufunguo wa kufungulia hazina za vitabu ni kusoma. Mtu yeyote awezaye kusoma huweza kuingia katika hazina hii akachukua akili na elimu nyingi kama awezavyo kuona.

Shaaban Robert "Vitabu" katika *Insha na Mashairi* (1967), uk. 54.

## 1.0 Utangulizi

Makala haya yamekusudiwa kujadili suala la utamaduni wa usomaji katika Tanzania, katika muktadha wa Kampeni ya Usomaji inayofanywa hivi sasa na Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania. Lengo letu ni kutathmini hali ya usomaji katika nchi yetu, matatizo yanayokwamisha juhudi za kujenga utamaduni wa usomaji, na namna ya kuyakabili. Lakini kabla ya hayo tutaangalia kwanza historia fupi ya uandishi na usomaji katika Tanzania kuanzia zama za kuingizwa kwa hati ya Kiarabu (karne ya 10) hadi leo.

## 1.1 Maana na Umuhimu wa "Utamaduni wa Usomaji"

Kusoma na kuandika ni mbinu za kurahisisha, kufanikisha na kudumisha mawasiliano. Neno "mawasiliano" hapa lina maana ya upashanaji wa taarifa. "Usomaji" unaelezwa na wataalamu kuwa *ni kitendo cha kutambua na kufasili alama zilizoandikwa au kupigwa chapa.*

Utamaduni wa usomaji ni mtindo wa maisha unaotawaliwa na maandishi katika viwango vyote - kiwango cha mtu binafsi na kiwango cha jamii nzima. Katika mtindo huo wa maisha, kusoma ni kama tendo la kimaumbile kama lile la kula au kuvuta pumzi.

Umuhimu wa tendo la aina hiyo haueleweki haraka kwa mtu wa kawaida hadi hapo anapovikosa vitu hivyo. Kwa mfano, sote huichukulia hewa ya uhai

(oksijeni) kama kitu cha kawaida tu, lakini kama tungeikosa hewa hiyo kwa dakika moja tu tungetambua haraka thamani yake isiyokadirika.

Mtu asiyejua kusoma ni sawa na mtu anayetembea gizani bila taa. Hili linadhihirika zaidi katika zile nchi zenye utamaduni wa kusoma. Katika nchi hizo, maisha ya mtu tangu asubuhi na mapema hadi anapopanda kitandani kulala usiku hutawaliwa na kuongozwa na kitendo cha usomaji. Mtu hawezi kunawa, kupika, kula chakula, kupanda basi, kujua njia, kununua vitu dukani, kufanya kazi ya ujira na pengine hata ya binafsi, na kuwasiliana na ndugu na wafanyakazi wenzake bila kujua kusoma na kuandika. Nchi yoyote ambayo imefikia hatua hiyo tunasema ina utamaduni wa usomaji. Hivyo utamaduni wa usomaji ni zaidi ya kusoma vitabu na magazeti.

## 2.0 Historia fupi ya Utamaduni wa Usomaji Tanzania

### 2.1 Kabla ya ukoloni

Usomaji nchini Tanzania ulianza mapema kidogo, kama miaka 1000 iliyopita. Tangu mwanzo usomaji na usomi ulifungamana na dini, kwanza Uislamu, baadaye Ukristo. Hivyo uandishi na usomaji ulianzia Pwani, ambako dini ya Kiislamu ilianza kuenea karne ya 10. Waarabu walioleta Uislamu walileta pia hati ya maandishi ambayo baadaye ilitumika kuandikia Kiswahili.

Aidha wenyeji waliosilimu waliwajibika kujifunza kusoma na kuandika Kiarabu katika madrasa ya dini ili waweze kujisomea wenyewe msahafu wa dini yao. Kwa njia hii, ujuzi na tabia ya kuandika na kusoma ilianza kuenea miongoni mwa Waswahili waliosilimu. Hivyo kufikia mwaka 1500 fasihi andishi ya Kiswahili ilikuwa imekwisha ota mizizi. Miongoni mwa maandishi ya mwanzo ambayo bado yapo ni

(a) *Swifa ya Mwana Manga* (utenzi unaodaiwa kutungwa na Fumo Liyongo) (1531).
(b) *Utendi wa Hamziyya* (Sayyid 'Aidarus bin Uthman 1652)
(c) *Siri 'lAsirari* (Binti Lemba, 1663)
(d) *Utendi wa Tabuka (Tambuka)* (Mwengo bin Athumani 1728)

*Swifa ya Mwana Manga* ni utungo wa kumsifu mwanamke. Siri 'lAsirari ni kisa cha kubuni; *Hamziyya* ni tafsiri ya utenzi wa zamani wa Kiarabu unaomsifu Mtume Muhamadi. *Tabuka* ni utendi juu ya vita kati ya Waislamu wa mwanzo na Mfalme Herekali wa dola ya Warumi. Tungo zote hizi ziliandikwa Kenya, japo bila shaka zilisomwa pia na Waswahili wa Tanzania.

Mbali na maandiko ya tarihi na historia (k.m. *Tarihi ya Kilwa* "Kilwa Chronicle" ya kama mwaka 1520), tungo za kifasihi za Kitanzania za wakati huo, kama zilikuwepo, sasa zimekwisha potea. Tungo za Kitanzania zinaanza kujitokeza kwa wingi zaidi katika karne ya 19, kwa mfano *Utenzi wa Ras 'lGhuli*

(Mgeni bin Fakihi wa Bagamoyo, kama 1855) na mlolongo wa tenzi za familia ya el-Buhry huko Tanga, yaani:

*(1) Utenzi wa Barasisi*
*(2) Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*
*(3) Utenzi wa Kadhi Kassim bin Jaafar*
*(4) Utenzi wa Seyyidna Hussein bin Ali*
*(5) Utenzi wa Abdirrahamani na Sufiyani*
(6) *Utenzi wa Vita vya Wadachi Kutamalaki Mrima, n.k.*

Tenzi hizi zilitungwa ili zighanwe au kutambwa misikitini na kwenye sherehe za kidini na kimila, hivyo ziliendeleza zaidi utamaduni wa kughani mashairi kuliko ule wa kusoma.

Kwa upande wa nathari, maandishi ya mwanzo katika hati ya Kirumi ambayo yalitokea kabla ya ukoloni yalielemea kwenye maeneo kadha tu, hasa:

(1) Tafsiri za vitabu vya Bibilia kwa Kiswahili ambazo zilifanywa na Wazungu walioingia Afrika Mashariki wakati huo. Tafsiri za mwanzo kabisa ni *Agano Jipya* na baadhi ya sura za *Agano la Kale* ziliyofanywa na Ludwig Krapf kati ya mwaka 1846 na 1848.
(2) Tafsiri ya kazi za fasihi ya Ulaya;
(3) Hadithi zinazotokana na fani za kimapokeo, k.m. ngano, visakale, n.k. (k.m. Steere *Swahili Tales* 1869)
(4) Hadithi za kimashariki ambazo tayari zilikuwemo katika fasihi simulizi ya Waswahili, k.m. *Abunuwas* na *Alfu-Lela-Ulela*;
(5) Sira au masimulizi kuhusu maisha ya watu mashuhuri;
(6) Historia kutokana na mapokezi ya wazee (k.m. Abdallah 'lAjjemy, *Habari za Wakilindi*, 1895);
(7) Masimulizi ya wasafiri (Velten Safari za Wasuaheli).

Maandiko hayo yalichapishwa vitabu na matbaa za Ulaya au za misheni, na ukoloni ulipoingia baadhi yalitumika shuleni hadi miaka ya Uhuru.

## 2.2 Kipindi cha Ukoloni

Maendeleo ya fasihi na usomaji nchini Tanzania wakati wa ukoloni yaliathiriwa na mambo matatu: elimu, hati ya maandishi ya Kirumi, na kuanzishwa kwa matbaa ya uchapaji wa vitabu na magazeti.

Elimu ya kikoloni iliambatana na alfabeti ya Kirumi. Elimu hiyo ilieneza lugha ya Kiswahili, Kidachi na baadaye Kiingereza katika maeneo ya bara kupitia shuleni. Kadhalika elimu hiyo ilieneza maarifa ya kusoma na kuandika, na maarifa ya kanuni za utunzi wa fasihi. Hati ya maandishi ya Kirumi ilienea kupitia elimu, pia kupitia makanisani, na ilianza kutumiwa na watunzi badala ya hati ya Kiarabu.

Stadi za kusoma na kuandika zilifundishwa kwa makini shuleni, na watoto wengi walihitimu shule za msingi, hasa darasa la nne au sita, wakiwa wanajua kusoma na kuandika vizuri. Miongoni mwa mbinu zilizotumika kuwazoeza wanafunzi kusoma ni:

(a) Maktaba za shule zenye vitabu vinavyohitajika na vinavyofaa kujisomea baada ya kutoka darasani;
(b) Maktaba za darasa (kabati) zinazosimamiwa na walimu wa lugha;
(c) Vipindi vya maktaba;
(d) Walimu kusimamia na kufuatilia shughuli za usomaji wa wanafunzi wao;
(e) ( e) Tunzo za usomaji;
(f) Magazeti ya shule au darasa, hususan magazeti ya ukutani yasiyo na gharama kubwa;
(g) Mashindano ya utunzi wa insha, mashairi, hadithi, n.k.
(h) Vyama vya hiari vya kutunga, kusoma na kujadili kazi za sanaa, hasa mashairi na hadithi;
(i) Vikundi vya maigizo.

Dosari kubwa ya mfumo huo wa kikoloni ni kwamba vitabu vingi vilivyosomwa vilisawiri mazingira ya kigeni mno, na vilikuwa na itikadi ya kutetea ukoloni, kumdhalilisha Mwafrika, na kueneza Ukristo.

Matbaa (karakana za kupiga chapa) yalisaidia kueneza vitabu na magazeti, na hivyo kuchipuza utamaduni wa kusoma. Matbaa ya mwanzo ni yale ya UMCA Press, Zanzibar, mwaka 1875; UMCA, Magila Press, mwaka 1905, na Government Printer, Zanzibar, mwaka 1892. Serikali ya Kidachi pia iliweka matbaa yake Dar es Salaam na Tanga.

Magazeti mengi yalichapishwa kwa lugha ya Kiswahili na kusambazwa; k.m. *Msimulizi* (1888), *Habari za Mwezi* (1894), *Pwani na Bara* (1910), *Rafiki Yangu* (1910), *Baraza* (1910) na *Mambo Leo* (1923). Yote isipokuwa Mambo Leo yalikuwa ni ya madhehebu ya Kikristo. Watunzi wengi, hasa wa mashairi, walipata umaarufu wao kupitia magazeti hayo, hasa Mambo Leo. Baadhi yao ni Shaaban Robert (1909-1962), Mdanzi Hanassa (k.1880-1952), Mzee Waziri (Kijana)(1900-1978), Mahmoud Hamdouny (Jitu-Kali)(1920-1997), Salehe Kibwana (k.1887-1966), Mwalimu Mwalimu Kihere (k.1903-1974), Ali bin Hemed, n.k. Uchapishaji wa vitabu ulipoanzishwa ulisaidia kuikuza na kuieneza sanaa ya ushairi, hasa baada ya shirika la EALB kuanzishwa mwaka 1948. Baadhi ya watunzi mashuhuri wa miaka hiyo (Mnyampala, Akilimali Snow-White, Amri Abedi, n.k.) walichapishiwa diwani zao na shirika hilo.

Njia nyingine waliyoitumia wakoloni kupata vitabu zaidi ni tafsiri. Kazi za fasihi ya Kizungu zilianza kufasiriwa kwa Kiswahili kuanzia miaka ya 1880 ( k.m. C. Kingsley *Mashujaa: Hadithi za Wayunani* 1889). Wakati wa ukoloni zilifasiriwa kazi nyingi zaidi za kigeni, mathalan: H.R. Haggard *Mchawi* (mfasiri

M.M.B. UMCA 1900); Neale *Nyumba ya Aptonga (The Farm of Aptonga)* (S.P.C.K, London 1924); Bunyan, J *Safari za Msafiri (Pilgrim's Progress)*, (S.P.C.K, London 1925); Johnson, F na Brenn, E. W (Waf.) *Alfu-Lela-Ulela* (labda kutoka katika lugha ya Kiingereza, London 1928); *Hekaya za Abunuwas* (mfasiri S. Chiponde, Macmillan 1928); R.L Stevenson *Kisiwa Chenye Hazina* (Mf. F.Johnson, Longman 1929); R. Kipling *Hadithi za Maugli* (Mf. F. Johnson, London 1929); R. Haggard *Mashimo ya Mfalme Sulemani* (Waf. Brenn na F. Johnson, Sheldon 1929) na *Hadithi ya Alan Quartermain* (Mf. F. Johnson, Sheldon 1934); N. Swift *Safari za Gulliver* (mf. F. Johnson, Sheldon, mwaka 1932); L. Carroll *Elisi katika Nchi ya Ajabu* (Mfasiri: E.V. St. Lo. Conan-Davies (Sheldon 1940); Wyss, J.R *Jamaa Hodari Kisiwani (Swiss Family Robinson)* (Mf. D. Diva London 1951); na D. Defoe *Robinson Kruso na Kisiwa Chake* (EALB k.1962). Kazi nyingine muhimu ziliyofasiriwa ni baadhi ya tamthiliya za William Shakespeare, k.m. *Mfanya Biashara wa Venisi* katika mtindo wa nathari (Taz. *Hadithi za Kiingereza,* Sheldon, 1940).

Kazi hizi, pamoja na nyingine zilizoigwa kutoka Ulaya, ndizo zilizosomwa kwa Kiswahili na Watanzania kipindi chote cha ukoloni hadi miaka ya 1940 na 1950, kazi zilizoandikwa na Watanzania wenyewe zilipoanza kutokea kwa wingi kiasi. Waandishi wa mwanzo wa Tanzania, k.m. Shaaban Robert, waliathiriwa na kazi hizi za tafsiri.

Mbali na tafsiri, palikuwa na maandiko machache ya kinathari ya Waswahili wenyewe, hususan maandishi ya tarikh za miji mbalimbali, *Safari za Waswahili, Maisha ya Hamed bin Muhammed (Tippu Tip)*, na *Habari za Wakilindi*, kama tulivyoeleza kabla. Maandishi haya yaliweka msingi wa mikondo na mitindo ambayo watunzi wa baadaye waliifuata.

Baada ya Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki kuanzishwa mwaka 1930, uandishi katika lugha ya Kiswahili ulihimizwa kwa njia ya mashindano. Kutokana na mashindano hayo, riwaya ya kwanza ya Kiswahili, *Uhuru wa Watumwa* (James Mbotela k.1885-1976), ilichapishwa mwaka 1934. Baadhi ya riwaya zilizotoka baadaye, kwa mfano M.S. Abdulla *Mzimu wa Watu wa Kale* (EALB 1960), na Faraji Katalambula *Simu ya Kifo* (EALB 1965) zilitokana na mashindano ya utunzi yaliyoendeshwa na kamati hiyo.

Miaka thelathini iliyofuata baada ya *Uhuru wa Watumwa* ilitawaliwa na kazi za Shaaban Robert (1909-1962). Riwaya yake ya kwanza, *Utubora Mkulima* (Nelson 1968) yasemekana ilitungwa mwaka 1946, lakini haikuchapishwa hadi mwaka 1968. Riwaya iliyofuata ni *Kufikirika* (OUP 1968) iliyoandikwa mwaka 1947, na kuchapishwa mwaka 1967. Riwaya ya tatu, *Kusadikika* (Nelson 1951) ilichapishwa mwaka 1951, na ya nne, *Adili na Nduguze* (Macmillan 1952) ilichapishwa mwaka 1952. Riwaya yake ya mwisho, *Siku ya Watenzi Wote* (Nelson 1968) iliandikwa kama 1960-62 na kuchapishwa mwaka 1968.

Mtunzi mwingine mashuhuri wa riwaya wa kipindi hicho ni Aniceti Kitereza (1896-1981), ambaye riwaya yake ya *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na*

*Ntulanalwo na Buhliwali* iliandikwa kwa lugha ya Kikerebe mwaka 1945, lakini haikupata mchapishaji hadi miaka ya 1970. Ilichapishwa kwa lugha ya Kiswahili na TPH mwaka 1981.

Shirika la Uchapishaji Vitabu la Afrika Mashariki (EALB) lilianzishwa mwaka 1948 ili kushughulikia uchapishaji wa vitabu kwa lugha za kienyeji. Shirika hilo lilipewa muhuri wa ithibati, yaani muhuri wa kudhibiti maandishi, na kati ya 1948 na 1960 lilichapisha karibu vitabu tofauti tofauti 1000 katika lugha 16 za Afrika Mashariki kwa ajili ya shule na wasomaji wa kawaida. Miongoni mwa vitabu hivyo, zilikuwemo hadithi, visa, tamthiliya na diwani za ushairi.

Shughuli za siasa za kudai uhuru zilipopamba moto kwenye miaka ya 1950-1960 utamaduni wa kusoma nao ulipamba moto; watu walitaka kujua maendeleo ya mapambano ya kudai uhuru kupitia katika magazeti ya Kiswahili na kilugha, k.m. *Mwafrika, Bukya na Gandi, Sauti ya TANU,* n.k. Aidha, watunzi wa fasihi, hasa washairi, walitunga tungo za siasa kwa wingi ili kuendeleza mapambano hayo. Tungo hizo zilichapishwa katika magazeti. Baadhi ya watunzi hao ni Mdanzi Hanassa, Salehe Kibwana, Mwalimu Mwalimu Kihere, Saadani Kandoro, Kaluta Amri Abedi, G. Pacha, Saidi Ludete, na Mwalimu J.K. Nyerere.

### 2.3 Baada ya Uhuru

Baada ya Uhuru, usomaji uliendelezwa katika muktadha wa siasa ya ujamaa na utaifa iliyotawala wakati huo. Mbinu zilizotumiwa na serikali ya chama kimoja iliyokuwepo ni kupanua elimu ya msingi na elimu ya watu wazima, kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili, kuunda asasi za uchapishaji na usambazaji wa vitabu, na kuweka ukiritimba wa utoaji na usambazaji wa vitabu vya shule.

Miaka ya 1960 na 1970 ilitumika kuweka misingi ya utaratibu mpya wa elimu. Siasa ya elimu ya kujitegemea ilitangazwa mwaka 1968. Elimu ya msingi kwa wote (UPE) ilitangazwa mwaka 1974. Juhudi za kuendeleza kisomo zilipamba moto sana kuanzia mwaka 1970. Kufikia miaka ya 1980 iliripotiwa kuwa asilimia 80 ya Watanzania walikuwa wanajua kusoma na kuandika. Ukuzaji wa Kiswahili ulitiliwa nguvu kwa kukitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa mwaka 1962, kuanzisha Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili mwaka 1964, na Baraza la Kiswahili la Taifa mwaka 1967. Uchapishaji ulitiliwa nguvu kwa kuanzishwa Shirika la Uchapishaji Vitabu la Tanzania (TPH) mwaka 1966, na Shirika la Vifaa vya Elimu Tanzania mwaka 1964. Ili kupata katarasi za kutosha kulingana na upanuzi wa elimu na shughuli za uchapishaji, kiwanda cha karatasi cha Mgololo kilianza kutengenza karatasi miaka ya 1980.

Juhudi hizo za kupanua elimu na usomaji ziliambatana na juhudi nyingine za kubomoa utaratibu wa kielimu ulioachwa na wakoloni. Kwa upande wa usomaji, mbinu za wakoloni za kuendeleza usomaji ziliachwa, ama makusudi, ama kwa sababu ya kutokuwa na vifaa, walimu na mazingira yanayofaa.

Hali ngumu ya uchumi miaka ya 1970, iliyoambatana na kuvunjika kwa

Jumuiya ya Afrika Mashariki (1977), Vita vya Kagera (1978-79) na sera hafifu ya uchumi, ilikwamisha zaidi shughuli za utoaji elimu, uchapishaji na usambazaji wa vitabu. Mashirika makubwa ya wazawa ya utoaji vitabu Afrika Mashariki wakati huo, EALB na EAPH, yalivunjwa au kuvunjika. Mali za baadhi ya mashirika hayo zililiwa au kusambaratishwa. Waandishi walipoteza haki zao. Mashirika ya kigeni yalipunguza shughuli zao au yalihama kabisa baada ya kupoteza soko la shule. Magazeti mengi ya binafsi yalikufa, na ya Chama Tawala na serikali yalidumu kwa sababu ya ukiritimba. Hivyo kufikia mwaka 1985 kiwango cha elimu na usomaji nchini kilikuwa kinazidi kushuka kwa kasi sana. Utamaduni wa usomaji ulidorora zaidi.

Pamoja na hali hiyo ngumu ya kiuchapishaji, kipindi cha 1960-85 kilishuhudia kujitokeza kwa waandishi wengi bora wa fasihi ya Kiswahili. Baadhi yao ni Ebrahim Hussein, Euphrase Kezilahabi, Penina Mhando, Mohamed Said Mohamed, Shafi Adam Shafi, M.S. Abdulla, C. Mung'ong'o, n.k. Fasihi ya Tanzania ilikua na kupevuka, japo ilikwamishwa na ugumu wa uchapishaji na usambazaji.

Miaka ya 1990 juhudi za kufufua uchapishaji na usomaji zilianzishwa na wahisani mbalimbali kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Utamaduni. Juhudi hizo ni pamoja na miradi ya ununuzi wa vitabu vya shule kutoka kwa wachapishaji wenyeji (na wageni) (PPP, IDA, PEP, CODE, English Support, n.k.). Miradi hii zaidi ilielekeza juhudi zake kwenye shule.

Mradi ambao ulilenga zaidi katika kuendeleza uchapishaji na usomaji wa vitabu vya ziada na vya burudani ni Mradi wa Vitabu vya Watoto (CBP). CBP ilianzishwa mwaka 1991, na kufikia wakati huu mradi umekwisha wezesha uchapishaji wa zaidi ya vitabu 110 vya kujisomea, umeendesha kozi nyingi za uandishi, uhariri, uchoraji na uchapishaji, na umesaidia kuanzisha vyama vya waandishi vya kanda. Hivi sasa CBP uko katika awamu yake ya pili, ambayo imejiwekea lengo la kuendesha kampeni ya usomaji (mbali na malengo yake ya awali). Labda huu ndio mradi pekee ambao umejipa jukumu la kukuza usomaji nchini. Ili juhudi zake zizae matunda, Mradi utahitaji kuungwa mkono kwa kila njia na asasi nyingine za jamii na seriakali.

### 3.0 Hali ya Usomaji nchini Tanzania Leo

Tunapozichunguza nchi zote zilizofanikiwa kujenga utamaduni wa usomaji, tunaona kuwa mafanikio yao yalitegemea sana hali na mahitaji ya kiuchumi, kisiasa na kitamaduni yaliyojitokeza kihistoria. Nchi hizo hazikujenga utamaduni wa kusoma kwa sababu tu ya kushabikia vitabu, bali kwa nia ya kukidhi haja muhimu ya kijamii. Baadhi ya mambo yaliyoathiri kuchipuka na kukua kwa utamaduni wa usomaji katika nchi hizo ni hali ya uchumi, hali ya utamaduni, hali ya kidemografia, hali ya lugha, hali ya kisomo na hali ya elimu. Aidha, hali ya sekta ya vitabu na hali ya kisiasa au kiutawala nayo pia iliathiri usomaji nchini.

Katika sehemu hii, tutaangalia mambo hayo manane katika muktadha wa Tanzania ili kuona yanaathiri vipi utamaduni wa usomaji.

### 3.1 Uchumi

Uchumi unapofikia kiwango fulani hudai ujuzi wa kusoma na kuandika. Uchumi wa namna hiyo huko Ulaya ulifikiwa wakati wa mapinduzi ya viwanda (karne ya 18/19). Uchumi wa kibepari uliozuka wakati huo ulihitaji wafanyakazi wenye kiwango fulani cha elimu.

Hali ya uchumi vilevile ndiyo inayochipuza hadhira ya wasomaji. Hadhira hiyo sharti iwe na utamaduni wa kusoma na uwezo wa kununua vitabu na magazeti. Hadhira ya aina hiyo ilijitokeza huko Ulaya kuanzia mwishoni mwa karne ya 18. Hapa kwetu, hadhira ya wasomaji ndio kwanza inachipuka, hasa baada ya kupanuka kwa kisomo chenye manufaa na elimu ya msingi kwa wote (UPE). Kipingamizi kikubwa kuhusu hadhira ya wasomaji hapa Tanzania ni kwamba hadhira hiyo ina ujuzi wa kusoma, lakini haina uwezo wa kununua vitabu na magazeti, na hakuna sera ya kuvifikisha vitu hivyo kwao kwa bei inayolingana na kipato chao. Katika nchi zilizokuwa za kisoshalisti, hasa Urusi, China na Kuba, upanuzi wa kisomo uliambatana na utoaji wa vitabu na machapisho mengi kwa bei rahisi ili kukidhi kiu ya watu ya kujisomea.

Yasemekana kuwa Tanzania ni nchi ya pili kwa ufukara duniani, na hali ya uchumi wake inazidi kudidimia. Uchumi wa Tanzania unategemea kilimo cha jembe la mkono, hakuna viwanda vya maana, uzalishaji uko chini, na kipato cha wastani hakifikii dola 200 za kimarekani kwa mwaka. Idadi kubwa zaidi ya watu hawana maji ya bomba wala nishati ya umeme vibandani mwao. Sera za wanasiasa mara kwa mara zimefanya hali ya uchumi iwe mbaya zaidi. Hali hii imeathiri sekta zote, zikiwemo sekta za elimu na uchapishaji. Ni vigumu kwa watu wanaoishi katika hali ya namna hii kuwa wasomaji wazuri, kwani, licha ya kukosa mazingira mazuri ya usomaji, hata uwezo wa kununua vitabu na magazeti hawana. Kusoma katika hali ya namna hii kunaweza kuwa adhabu badala ya kuwa burudani. Hivyo hali ya uchumi bado ni kikwazo cha usomaji hapa Tanzania.

### 3.2 Utamaduni

Katika nchi za Kiislamu, utamaduni wa kusoma Kiarabu ni sehemu ya mila ya dini. Ujuzi wa kusoma na kuandika ambao waumini wengi waliupata katika madrasa baadaye ulitumika katika nyanja nyingine za maisha. Huko Ulaya, mila ya kusoma ili kujipatia maarifa ilikuwepo tangu kale kwa kundi la wateule, hasa watawa na mapadre, wa dini, na wasomi wengine, lakini utamaduni wa kusoma umezuka pamoja na ubepari wa viwanda. Hapa kwetu, isipokuwa katika sehemu za Pwani na Visiwani, mila ya kusoma ni zao la ukoloni, na utamaduni wa kusoma bado haujajengeka. Bado inawezekana kwa Mtanzania wa wastani kuishi kwa furaha bila kugusa kitabu au gazeti au hata barua.

Utamaduni wa Tanzania, kama utamaduni wa nchi nyingi za Afrika, bado ni wa kikulima au kiujimaujima unaowashuku "wasomi". Henry Chakava (1996:95) ameeleza vizuri kuwa katika lugha nyingi za Kiafrika, neno "msomi" lina maana ya "Mkristo", yaani mtu aliyeacha dini na utamaduni wake wa asili na kujiunga na dini na utamaduni wa wageni wa Kizungu. Waganda wamekwenda mbele zaidi na kuhuusisha "usomi" na usaliti katika msemo wao wa *Si Muganda musomi* (Si Mganda ni msomi). Kwa upande wa Tanzania, Nyerere aliieleza vizuri hali hii aliposema:

"I think we have to try very hard in Tanzania to cultivate the habit of reading among our young people and among our newly literate citizens. It is a fact which we must recognize, that in dealing with the modern world children in Europe have two big advantages over our own children. One is the familiarity with mechanical things; the other, and perhaps even more important one, is familiarity with books. Too often in our own society a person who sits down to read is accused of being lazy or of being unsociable. This attitude we must change. When we get to the position where a man and wife can sit together in the evening each reading or reading to each other, and when their children are encouraged to learn out of school by reading books which are easily available, then we shall have made a big break-through in our development...."

J.K. Nyerere "The Importance and Pleasure of Reading" katika *Freedom and Socialism* (OUP Dar es Salaam 1968), uk.108.

Kwa ufupi, kwa mtazamo wa wengi katika utamaduni wetu, mtu anayependa kusoma sana anaonekana ni mbinafsi, asiyependa ushirikiano, na "mchawi". Huu ni mtazamo ambao inabidi tupambane nao, na huenda kampeni hii ikasaidia katika kuubadilisha.

### 3.3 Demografia

Idadi ya watu wa kundi moja, wenye kuzungumza lugha moja na wenye kuishi mahali pamoja vilevile huweza kuamua hali ya usomaji katika jamii fulani. Watu wa jamii fulani wakiwa wachache mno huenda wakashindwa kuendeleza usomaji katika lugha yao wenyewe kwa sababu ya ugumu wa kupata waandishi na kutoa machapisho ya kutosha.

Idadi ya watu ni muhimu katika kuendeleza uchapishaji. Kwa hapa Tanzania, hilo si tatizo kwa kuwa tunao watu wa kutosha wenye kuzungumza lugha moja (Kiswahili) wanaoweza kuwa soko kubwa la vitabu na magazeti. Takwimu zisizo rasmi zinaonyesha kuwa Watanzania hivi sasa wanafikia milioni 30.

### 3.4 Lugha

Maandishi yoyote yale huwakilisha lugha fulani. Hivyo usomaji hufungamana na lugha. Katika nadharia ya kufundisha kusoma, inaelezwa kuwa mtoto ambaye

hana umilisi wa lugha ya kufundishia, mathalan ana msamiati mdogo mno, wakati anapoanza shule, hupata shida sana kujifunza kusoma, na anaweza hata asifanikiwe kuwa msomaji mahiri. Kadhalika, lugha haiwezi kujenga usomaji iwapo haina hati ya maandishi (alfabeti), na haizungumzwi na watu wengi. Hivyo, jamii ndogo ndogo zenye lugha nyingi tofauti bila kuwa na lugha moja au mbili zinazowaunganisha haziwezi kuwa na utamaduni imara wa usomaji. Aidha, ni vigumu kujenga tabia na utamaduni wa usomaji kwa kutegemea lugha ya kigeni, kwani si watu wote (au walio wengi) watakaoweza kuimudu lugha hiyo vizuri.

Tanzania ina bahati ya kuwa na lugha moja inayowaunganisha Watanzania wote, ambayo ni Kiswahili. Hivyo msingi wa kiisimu wa kujenga utamaduni wa usomaji tayari upo. Aidha, baadhi ya lugha zetu za kikabila zina wazungumzaji wa kutosha (zaidi ya milioni moja) kuweza kuendeleza uandishi na usomaji katika lugha hizo. Mifano ni lugha kama Kisukuma/ Kinyamwezi, Kichagga, Kihehe, Kiyao, Kigogo, Kiha, Kihaya/Kinyambo, n.k.

Tutake tusitake, kwa hapa Tanzania Kiswahili ndicho chombo kikubwa cha usomaji, na lazima kampeni ya usomaji ielekezwe hapo. Lugha za makabila zinaweza kutumika katika magazeti na vitabu pale inapowezekana. Lugha za kigeni kama Kiingereza na Kiarabu vilevile zinafahamika kwa baadhi ya Watanzania, hivyo hizi pia zinaweza kutumika kuendeleza usomaji miongoni mwa hao wachache wanaozifahamu.

### 3.5 Kisomo

Utamaduni wa usomaji hufungamana na ujuzi wa kusoma. Jamii yenye asilimia kubwa ya watu wajuao kusoma (angalao zaidi ya 50%), ndiyo inayoweza kujenga utamaduni wa usomaji. Hivyo hatua ya kwanza kabisa ya kujenga utamaduni huo ni kueneza kisomo (kwa watu wazima) na elimu ya msingi (kwa watoto wote).

Kisomo ni ujuzi na uwezo wa kusoma na kuandika. Bila ujuzi huo kampeni ya usomaji itagonga ukuta. Juhudi za Tanzania za kuendeleza kisomo chenye manufaa miaka ya 1970 ziliwawezesha asilimia 80 ya Watanzania kujua kusoma na kuandika. Baadhi ya watu hao sasa wamekwisha sahau stadi hiyo kutokana na kukosa vitabu na majarida ya kujisomea. Hivyo, ingawa hali ya kisomo hapa Tanzania ni nzuri, lakini bado vinahitajika vitabu vizuri vinavyowafaa wasomaji wa kiwango hicho ili kuwazoeza kusoma wasije wakasahau.

Vitabu vya watu wazima wa kiwango hicho vinatakiwa viwe ni vifupi (kwa vile wanakisomo hawajapata uzoefu wa kusoma matini marefu); viwe sahili (rahisi) kimuundo (ili vieleweke kwa urahisi kwa walengwa); viwe na lugha rahisi (msamiati mwepesi, sentensi fupi fupi); na maudhui yake yawe sahili lakini ya kiwango cha watu wazima (yahusu maisha na matatizo yao ya kila siku).

Miaka ya 1970 vilikuwepo vijitabu vingi vya aina hiyo. Mfano mzuri ni vitabu vya Shaaban K. Msuya: *Mazungumzo ya Mchana* (TPH 1973), *Mazungumzo ya Usiku* (TPH 1975), *Mazungumzo ya Jioni* (TPH 1976),

*Tuzungumze Yajayo* (BSA 1978) na *Siri ya Bahati* (BSA 1978). Hivi leo vitabu hivyo havipatikani tena, na baadhi vina maudhui yaliyopitwa na wakati. Hivi hili ni eneo ambalo linahitaji kutiliwa mkazo katika kuendeleza uandishi na usomaji.

### 3.6 Elimu

Kiwango cha wastani cha elimu katika taifa lolote ni kigezo kikubwa cha usomaji. Katika nchi nyingi zilizoendelea, watu waliohitimu elimu ya chuo kikuu wanazidi 70%. Katika Tanzania, wahitimu wa chuo kikuu hawafikii 1%. Waliohitimu elimu ya sekondari pia hawazidi 15%. Kwa kuwa elimu husaidia kujenga tabia ya usomaji, ni wazi kuwa bado tuna kazi kubwa ya kufanya ili kuwa na watu wenye kiwango cha elimu kinachowaruhusu kuwa wasomaji mahiri kitabia.

### 3.7 Sekta ya Vitabu

Sekta ya vitabu hujumuisha maeneo yafuatayo: uandishi, uchapishaji, uchapaji, upatikanaji wa karatasi na vifaa vya uchapaji, usambazaji wa vitabu, mfumo wa maktaba. Nchi zenye utamaduni wa usomaji vilevile zina sekta ya vitabu iliyokomaa. Zina waandishi wengi na wazuri, wachapishaji wapo, wachapaji ni wengi na wana mashine na vifaa vya kisasa, karatasi hupatikana bila shida, mfumo wa usambazaji upo na unafanya kazi - maduka ya vitabu yapo hadi vijijini, maktaba ni nyingi na zimejaa wasomaji, n.k. Takwimu za UNESCO (taz. Kiambatisho) zinathibitisha hoja hii. Takwimu hizo zinaonyesha kuwa kwa mwaka nchi ndogo ya Sweden inatoa karibu idadi sawa ya machapisho (titles) na bara zima la Afrika (k.m. mwaka 1990 Sweden ilitoa vitabu 12034 na Afrika ilitoa vitabu 13,000).

Tanzania haina upungufu wa waandishi wa vitabu. Vyama vya waandishi pekee vina wanachama wanaofikia 500. Wapo waandishi wengi pia ambao si wanachama wa vyama hivyo. Miswada inayoandikwa na watunzi hao na kukosa wachapishaji ni mingi sana. Tatizo la ujuzi wa mbinu za uandishi lipo, lakini lingeweza kupatiwa ufumbuzi kama sekta nzima ya uchapishaji ingekuwa inafanya kazi ipasavyo.

Waandishi wanakabiliwa na tatizo la kutothaminiwa na serikali, wachapishaji na umma kwa jumla. Hili ni tatizo linalowakabili wasanii wetu wengi. Kwa mfano, hawapati haki zao za kimkataba kutoka kwa wachapishaji walio wengi, vitabu vyao havifanyiwi mapitio, n.k. Mfano mzuri wa namna waandishi wanavyodhalilishwa ni tukio la sherehe za BAKITA za "Siku ya Kiswahili" mwaka 1995. Katika sherehe hizo, waandishi wa vitabu walioshinda tunzo walipewa vyeti tu na kunyimwa tunzo zao za fedha. Haijaelezwa nani alipokea fedha hizo "kwa niaba yao"!

Tatizo kubwa liko upande wa uchapishaji wa vitabu. Hali ya uchapishaji hapa Tanzania inakatisha tamaa. Ingawa wachapishaji waliosajiliwa wanazidi 150, lakini wachapishaji wa kweli wa kibiashara hawazidi 40. Kati ya hao, labda

wachapishaji kama 10 ndio hutoa angalao kitabu kimoja kila mwaka (mbali na vitabu vya kiada na vya Mradi wa Vitabu vya Watoto). Wachapishaji wa kigeni (Macmillan, Longman, Oxford, Nelson, n.k.) waliihama Tanzania wakati wa Ujamaa, au walibakiza ofisi ndogo za mauzo tu. Mashirika makubwa yaliyoanzishwa Afrika Mashariki ambayo hayakuwa ya dini, yaani EALB na EAPH yaliporomoka miaka ya 1980. TPH vilevile linalegalega, na kuna mipango ya kuliuza. DUP limekuwa mahtuti kwa kipindi kirefu, na juhudi za kulifufua bado hazijaonyesha matunda mazuri. Hivyo tumebakiwa na wachapishaji wadogowadogo wa binafsi, ambao uwezo wao wa kutoa vitabu pia ni mdogo, na wachapishaji wakubwa wa kidini, k.m. Ndanda-Peramiho Mission Press, Inland Press, TMP Tabora, n.k. ambao malengo yao yanaelemea upande wa dini zaidi. Wapo pia wachapishaji wachache wa vitabu vya Kiislamu.

Matatizo makubwa yanayowakabili wachapishaji yanaelezwa na PATA kuwa ni:

(1) Sera ya ukiritimba wa vitabu vya kishule iliyofuatwa na Wizara ya Elimu tangu miaka ya 1970;
(2) Ukosefu wa soko na maduka ya kuuzia vitabu, hasa baada ya sera ya ukiritimba
kusababisha maduka mengi ya vitabu kufungwa;
(3) Ukosefu wa wataalamu wa taaluma ya uchapishaji;
(4) Ukosefu wa mtaji.
(5) Ukosefu wa wapiga chapa wazuri;
(6) Ukosefu wa vifaa vya kuchapia vitabu, hasa karatasi, wino, filamu na mitambo.

Baadhi ya matatizo haya yameanza kushughulikiwa kisera kuanzia katika miaka ya 1990. Kwa mfano, sera mpya ya Wizara inayofuta ukiritimba ilitangazwa mwaka 1992, na imeanza kutekelezwa kwa awamu. Tatizo la mitaji bado lipo, japo juhudi mbalimbali zinafanywa kulikabili. Tatizo la utaalamu linashughulikiwa kwa njia mbalimbali na CBP, PATA, UWAVITA, na asasi nyingine. Chuo Kikuu Huria pia kinatarajia kuanzisha kozi ya uchapishaji kama sehemu ya digrii yake ya Sayansi za Habari na Mawasiliano. Kwa upande wa uchapaji, wachapaji wadogowadogo wamejitokeza miaka ya 1990, na viwango vya upigaji chapa vimeanza kupanda. Hata hivyo, bado vifaa vingi ni adimu na vinanunuliwa kutoka nje ya nchi kwa gharama kubwa. Karatasi za Mgololo hazitoshelezi mahitaji, na ni hafifu.

Hali hii imesababisha utoaji wa vitabu, hasa vya kujisomea kwa ajili ya burudani na maarifa, ukwame. Utafiti tuliofanya mwaka 1996 ulionyesha kuwa katika kipindi cha miaka 10 (kati ya 1985-1995), wachapishaji 12 wa vitabu kwa pamoja walichapisha vitabu vya kifasihi visivyozidi 77, yaani wastani wa vitabu 7 kwa mwaka kwa ajili ya watu milioni 30! Na katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 1990, Maktaba Kuu ya Taifa ilipokea vitabu vipya 20 tu vya

fasihi! (Ni dhahiri kuwa takwimu hizi zinagongana kidogo na na takwimu za UNESCO (1993) zilizomo katika Kiambatisho).

Mbali na matatizo yaliyoelezwa, lipo tatizo la rushwa na kukosa uaminifu upande wa baadhi ya wachapishaji. Vitabu vingi vinatolewa nakala nyingi na kuuzwa kisirisiri bila waandishi kufahamishwa au kulipwa haki zao; mirabaha hailipwi kwa wakati, au hailipwi kabisa; ripoti za mauzo hazitolewi kwa waandishi, n.k. Hili ni tatizo la mashirika ya umma na ya binafsi pia. Kwa upande wa mashirika makubwa kama EALB na EAPH, mashirika hayo yalikufa kutokana na uroho wa baadhi ya watumishi na wakurugenzi wa mashirika hayo. Kwa mfano, fedha na mali za EAPH zililiwa huko Nairobi, na hapa Dar es Salaam haijulikani mali hizo zimeingia katika mikono ya nani!

Kwa upande wa magazeti, hali ni nzuri zaidi. Magazeti mengi yameanzishwa tangu mwaka 1990. Hivi sasa yapo magazeti na majarida zaidi ya 200, na kati yao zaidi ya 40 hutoka mara kwa mara. Hii ni hali ya kutia moyo, kwani kustawi kwa magazeti hayo ni dalili kuwa tabia ya usomaji imeanza kujengeka miongoni mwa wananchi. Kwa kuwa vitabu hakuna, magazeti kwa wakati huu ndiyo nyenzo kubwa ya utamaduni wa kusoma nchini Tanzania.

### 3.8 Siasa na Utawala

Hali nzuri ya kisiasa, yenye amani na demokrasia, husaidia kupalilia utamaduni wa usomaji. Katika nchi nyingi za Afrika, vurugu na zahama za mara kwa mara hukwamisha hata shughuli za utoaji vitabu na usomaji. Nchi isiyo na serikali (k.m. Somalia), au ambayo nusu ya raia wake ni wakimbizi, haiwezi kuwa na utamaduni wa usomaji. Bila kuwa na haki ya kuishi ni vigumu kuwa na haki ya kusoma. Kadhalika, nchi yenye utawala wa mabavu unaodhibiti vikali na kuchuja machapisho yanayotolewa kwa umma haiwezi kuwa na utamduni imara wa usomaji, maana utamaduni wa usomaji ni sehemu ya demokrasia.

Kwa upande wa Tanzania, kisiasa tumekuwa na amani na utulivu wa kiasi fulani tangu tupate uhuru. Hivyo mazingira ya kisiasa ya kuruhusu kuchipuka kwa utamaduni wa usomaji yalikuwepo. Kilichotukwamisha ni matatizo ya kisera na kiuchumi tuliyoyaeleza hapo juu. Hivi karibuni umeanzishwa mfumo wa vyama vingi vya siasa. Mfumo huo umesaidia kuleta msisimko katika shughuli za siasa, na bila shaka umechangia katika kuyapa umaarufu magazeti fulani. Kwa upande mwingine, mfumo huu usipoelekezwa katika njia nzuri unaweza kuzaa vurugu za kisiasa kutokana na tamaa ya baadhi ya wanasiasa ya kuhakikisha wanakuwa madarakani kwa kila hali, hata kama ni kwa njia ya kuchochea chuki za kikabila, kidini na nyinginezo. Hali hii isipodhibitiwa mafanikio kidogo yaliyopatikana katika kujenga utamaduni wa amani na usomaji huenda yakafutika.

## 4.0 Mambo ya Kufanya ili Kukuza Usomaji

Baada ya kueleza hali ya usomaji Tanzania na matatizo yenye kuathiri ukuaji wa

utamaduni wa kusoma hebu sasa tuangalie mambo ya kufanya ili kukuza usomaji. Ili kukuza utamaduni wa usomaji hapa nchini, hatua zifuatazo hazina budi kuchukuliwa kitaifa mintaarafu hali ya uchumi, utamaduni, lugha, kisomo, elimu, sekta ya vitabu na hali ya kisiasa na kielimu. Nitafafanua na kutoa mapendekezo kuhusu mambo ya kufanya kwa kila moja na wasomaji watatafakari mapendekezo mengine kulingana na uzoefu wao.

### 4.1 Hali ya Uchumi

Kubadili uchumi wa Tanzania ni suala la kisera lenye kuhitaji mwafaka wa kitaifa na mkakati wa muda mrefu. Si rahisi kutoa jibu hapa; kinachohitajika kufanywa ni kuwa na sera nzuri ya uwekezaji itakayojenga uwiano mzuri wa sekta zote za uchumi - kilimo cha kijadi na kilimo cha kisasa, viwanda vikubwa na viwanda vidogo, na sekta za huduma kama nishati, maji, njia za mawasiliano, elimu fedha na mabenki, n.k. Kama vyama vya siasa vingekubaliana juu ya suala hili vingelisaidia taifa zaidi kuliko ilivyo sasa.

### 4.2 Hali ya Utamaduni

Kubadili mazingira ya kitamaduni kunategemea maendeleo ya kiuchumi. Hata hivyo, kampeni ya kuwaelimisha watu kuhusu umuhimu wa kusoma, na kwamba wasomaji si "wachawi" inaweza kuanza kwa njia mbalimbali. Njia ya kudumu ya kubadili utamaduni huu ni kuwazoeza watoto kuwa wasomaji kuanzia udogoni katika shule za awali na za msingi ili wamalizapo shule waendelee na tabia hiyo.

### 4.3 Hali ya Lugha

Sera mpya ya utamaduni na lugha itekelezwe. Juhudi za ukuzaji wa Kiswahili kimsamiati ziendelee, na matumizi ya lugha hiyo yahimizwe na kupanuliwa zaidi. Visaidizi vya wasomaji na waandishi, k.m. makamusi, hazina za maneno (*Thesaurus*), programu za kompyuta, n.k. viandaliwe. Ili haya yatekelezwe ipasavyo, vyombo vya kukuza Kiswahili viimarishwe na kupewa watu na nyenzo za kuifanya kazi hiyo. Matatizo ya kiuongozi na kiutawala yanayovikabili vyombo hivyo, hususan BAKITA, yatafutiwe dawa.

### 4.4 Hali ya Kisomo

Kisomo chenye manufaa bado hakijapitwa na wakati. Hapa mambo mawili yanahitaji kufanywa:

(a) Kufufua au kuendeleza vituo vya kisomo kama ilivyokuwa miaka ya 1970;

(b) Kuhimiza uandishi na uchapishaji wa vitabu vya watu wazima waliohitimu kisomo, na kuhakikisha vinauzwa kwa bei watakayoimudu.

### 4.5 Hali ya Elimu

Mambo ya kufanya ili kukuza usomaji katika shule:

(a) Kuimarisha elimu ya msingi ili angalao mtoto anapohitimu awe anajua kusoma na kuandika vizuri;

(b) Kurejesha somo la maktaba na vipindi vya kujisomea katika ratiba za masomo;

(c) Kuanzisha au kufufua maktaba za shule;

(d) Kuanzisha au kufufua magazeti ya shule, yakiwemo yale ya ukutani.

(e) Kufundisha mbinu bora na za kisasa za kufundisha kusoma na kuandika kwa wakurufunzi wa ualimu katika vyuo vya walimu; na kuwapiga msasa (kwa njia ya semina na warsha) walimu ambao tayari wako kazini.

(f) Kuanzisha utaratibu wa mashindano ya utunzi na usomaji kwa watoto, na kutoa tunzo kwa wale wanaoshinda;

(g) Kuimarisha na kupanua utoaji wa vitabu vya watoto vya kujisomea kwa kusaidiana na CBP na asasi nyingine zinazoshughulikia suala hilo.

### 4.6 Hali ya Sekta ya Vitabu

(a) Juhudi za kufufua uchapishaji wa vitabu ambazo zimekwisha kuanza ziimarishwe kwa kuzingatia mahitaji ya wahusika wote katika sekta hiyo, yaani: waandishi, wachapishaji, wapiga chapa, wauza vitabu, maktaba na wasomaji.

(b) Uhusiano kati ya waandishi na wachapishaji uboreshwe; wawakilishi wa pande hizo mbili wakae pamoja kujadili uhusiano wao na kupeana maadili ya kufuata.

(c) Kuna haja ya kuwa na Mfuko Maalumu wa Usomaji utakaonunua vitabu au kufidia sehemu ya gharama za kutoa vitabu kwa ajili ya Kampeni ya Usomaji.

(d) Wizara ya Elimu iweke utaratibu mahsusi wa kununua na kusambaza vitabu vya CBP ili viwafikie watoto wote na viwe ni kianzio kizuri cha maktaba za shule.

(e) Sheria ya hakimilki idurusiwe ili ilingane na wakati uliopo.

(f) Tanzania itie sahihi mikataba ya kimataifa ya hakimilki.

### 4.7 Siasa na Utawala

(a) Vyama vya siasa na vikundi vingine vya kijamii vishirikiane kudai na kudumisha haki za msingi za kisiasa na kijamii, kukuza umoja wa kitaifa, kuendeleza lugha na utamaduni wa taifa katika sera na matendo yao, na kukataa ukabila na udini. Mwelekeo wowote wa kubana uhuru wa kupeana habari na maarifa kwa kudhibiti vyombo vya habari na fasihi upigwe vita.

(b) Usomaji katika Afrika Mashariki ulianza kwa kushirikisha nchi zote za Afrika Mashariki bila kujali mipaka. Ushirikiano huu ulivurugwa miaka ya 1970-1990 kwa sababu za kisiasa na za kibinafsi. Ni muhimu kwa watu wa Afrika Mashariki kurejesha ushirikiano huu wa usomaji, maana lugha tunazotumia ni zilezile (Kiswahili na Kiingereza), utamaduni wetu unafanana, na soko letu ni moja. Ushirikiano utarahisisha utoaji na usambazaji wa vitabu, na utasaidia kushusha bei za vitabu hivyo kwa kuwa vitatolewa nakala nyingi zaidi.

## 5.0 Tamati

Utamaduni wa usomaji bado ni mgeni hapa kwetu, bali hatuwezi kuukwepa kwa kuwa maisha ya karne ijayo yatatawaliwa na usomaji. Taifa la wasiosoma litaachwa nyuma na maendeleo ya historia. Hivyo yatubidi tuanze sasa kuujenga utamaduni huo.

Mwisho hatuna budi kusisitiza kuwa watekelezaji wa mambo yote tuliyoyapendekeza, na kampeni nzima ya usomaji, si serikali tu, bali ni sisi wote, yaani: vyombo vya serikali, asasi za hiari, walimu, wazazi, waandishi, wachapishaji, wauza vitabu, wakutubi, asasi za dini, na wanafunzi wenyewe.

## Marejeo


Altbach, P.G., (1992), *Publishing and Development in the Third World*, Vistaar Publications, New Delhi/Heinemann, Nairobi.

Bertoncini, E., (1989), *Outline of Kiswahili Prose Fiction*,. EJ. Brill, Leiden.

Bgoya, W (n.d.) "Books and Reading in Tanzania", *Studies on Books and Reading* No. 25. UNESCO, Paris.

Bgoya, W., (1992), "The Challenge of Publishing in Tanzania" in Altbach 1992: 169-190.

Chakava, H., (1983), "Books and Reading in Kenya", *Studies on Books and Reading* No. 13. UNESCO, Paris.

Chakava, H., (1996), "Publishing in Africa: One Man's Perspctive". *Bellagio Studies in Publishing* # 6 & EAEPL, Nairobi.

Harries, L., (1962), *Swahili Poetry*, OUP, Oxford.

Kabali, H., (1995), "Distribution and Selling of Books in Tanzania." Paper presented at the Round Table Discussion on Creative Writing and Publishing in Tanzania, Dar es Salaam, 12/12/95.

Kalugula, C and Read, A (n.d.), "A Report on Primary School textbook Provision and Availability in Tanzania: Current Problems and Key Issues." Unpublished Report.

Knappert, J. (1979), *Four Centuries of Swahili Verse*, Heinemann, London.

Minzi, L and Omari, B., (1994), "Study on the Distribution of Children's Books in Tanzania." Unpublished Report, CBP.

Mitchell, D.C., (1982), *The Process of Reading*, John Wiley & Sons, Chichester/New York.

Mlacha, S.A.K na Madumulla, J.S., (1991), *Riwaya ya Kiswahili*, DUP, Dar es Salam.

Mulokozi, M.M., (1989), "A Survey of Swahili Literature: 1970-1988" *Vinduet* 4: 46-51, Oslo.

Mulokozi, M.M na Mung'ong'o, C.G (Wah.), (1993), *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*,UWAVITA/DUP, Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M., (1993), *Survey of the Printing Industry in Eastern and Southern Africa*, IKR/UNESCO, 1993.

Mulokozi, M.M, (1996), "The State of Creative Literature and Publishing in Tanzania and Proposal for a Literature Support Project," HIVOS/UWAVITA, Dar es Salaam.

Nyerere, J.K., (1968), "The Importance and Pleasure of Reading" in *Freedom and Socialism*,Oxford University Press, Dar es Salaam, p. 108.

Pearce, D., (1990), "A Plan for a Children's Book Project Tanzania," CODE, Dar es Salaam.

Shaaban Robert, (1967), "Vitabu" katika *Insha na Mashairi*, Nelson, Dar es Salaam.

Strang, R and Bracken, D.K. (1957), *Making Better Readers*, D.C. Heath & Co, Boston.

TUKI, (1983), *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 2: Uandishi na Uchapishaji*, TUKI, Dar es Salaam.

TUKI, (1983), *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 3: Fasihi*. TUKI, Dar es Salaam.

UNESCO, (1993), *Statistical Yearbook*, Paris.

Whiteley, W., (1969) *Swahili: The Rise of a National Language*, Methuen, London.

**Kiambatisho: Jedwali**

*Jedwali la 1: Uchapishaji wa vitabu (titles) na magazeti duniani 1991*

| | Jumla ya titles | Titles kwa kila watu 1,000,000 | Idadi ya magazeti ya kila siku | Nakala kwa kila watu 1000 |
|---|---|---|---|---|
| Dunia | 863,000 | 160 | 7780 | 111 |
| Afrika | 13,000 | 20 | 170 | 17 |
| Amerika | 144,000 | 198 | 2950 | 153 |
| Asia | 215,000 | 70 | 2190 | 64 |
| Ulaya | 403,000 | 802 | 1659 | 245 |
| Urusi | 76,000 | 261 | 691 | 477 |

Chanzo: Unesco 1993

Jedwali la 2: Uchapishaji wa vitabu Afrika (nchi chache) mwaka 1990 (ukilinganishwa na uchapishaji ktk baadhi ya nchi ndogo za Ulaya na Amerika)

| Nchi | Vitabu Vyote | Vitabu vya kifasihi |
|---|---|---|
| Tanzania | 172 | 47 |
| Kenya | 348 | 23 |
| Zimbabwe | 349 | 56 |
| Afrika kusini | 4950 | 1066 |
| Kuba | 1858 | 426 |
| Sweden | 12034 | 3509 |
| Norway | 3712 | 1217 |

Chanzo: UNESCO 1993